

HALMASHAURI YA WILAYA YA GAIRO



Namba ya Zabuni LGA.143/2022-2023/NC/05

Kwa ajili ya utoaji wa huduma ya:

KUFANYA USAFI, KUTOA MCHANGA KATIKA MITARO NA BARABARA ZA LAMI NA KUFAGIA BARABARA ZA VUMBI, KUZOA TAKA NGUMU NA KUKUSANYA ADA YA USAFI

MWALIKO WA ZABUNI


Tarehe: 31/05/2022

1. Mwaliko huu wa zabuni unatokana na Tangazo la Jumla la Ununuzi (TJU) kwa ajili ya Halmashauri ya Wilaya ya Gairo kwa Mwaka wa fedha 2022/2023.
2. Halmashauri ya Wilaya ya Gairo inapenda kuwaalika watu Binafsi, Makampuni, Ushirika, Taasisi au Vikundi vya Watu vilivyosajiliwa kisheria wenye nia, uwezo na uzoefu wa kufanya kazi hiyo kwa kutuma maombi ya zabuni ya kufanya usafi, kutoa mchanga katika mitaro na barabara za lami na kufagia barabara za vumbi, kuzoa taka ngumu na kukusanya ada ya usafi katika Kata tatu ambazo ni Magoweko, Gairo na Ukwamani, kwenye eneo la Mamlaka ya Mji Mdogo Gairo kama ifuatavyo:-

S/Na	Nambari ya zabuni	Eneo/Mahali	Maelezo ya huduma	Tarehe ya kutembelea maeneo (Site visit)
1	LGA.143/2022-2023/NC/05	Kata za Magoweko, Gairo na Ukwamani (Eneo la Mamlaka ya Mji Mdogo Gairo)	Kufanya usafi, kutoa mchanga katika mitaro na barabara za lami na kufagia barabara za vumbi, kuzoa taka ngumu na kukusanya ada ya usafi	Tarehe: 7/6/2022 Muda: Saa 4:00 Asubuhi Mahali: Ofisi ya Mkurugenzi Mtendaji - Kitengo cha Usafi na Mazingira. Gharama: utajigharamia

3. Hivyo Halmashauri ya Wilaya ya Gairo inakukaribisha kuwasilisha zabuni kwa ajili ya utoaji huduma kama ilivyoelekezwa kwenye Jedwali hapo juu.
4. Zabuni hii inatangazwa kitaifa kwa kufuata taratibu za manunuzi zilizooneshwa katika Sheria ya Ununuzi ya Umma ya Mwaka 2011 na Kanuni zake za mwaka 2013 sambamba na marekebisho yake yote ya mwaka 2016.

5. Wazabuni wanaweza kupata taarifa na ufanunuzi zaidi na kupata nyaraka zabuni (Tendering documents) kwenye ofisi ya Katibu wa Bodi ya Zabuni, Halmashauri ya Wilaya ya Gairo, S.L.P 40, Gairo kuanzia saa 2:00 asubui hadi saa 9:30 alasiri kuanzia Jumatatu hadi Ijumaa isipokuwa siku za Sikukuu za Umma.
6. Nyaraka za zabuni zitapatikana kwa kulipia Ada ya Tshs. 30,000/= (Elfu **Thelethini tu**) ambayo haitarudishwa. Mwombaji atafika Ofisi ya Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Wilaya ya Gairo ili kupata "control namba" ya kulipia zabuni husika na hakikisha risiti ya malipo unaambatanisha.
7. Zabuni zote lazima ziambatanishwe na Tamko la Dhamana ya Zabuni (Tender securing Declaration) katika muundo (format) kama ilivyowekwa kwenye nyaraka ya zabuni.
8. Zabuni zote zijazwe kikamilifu kwa kuainisha Namba ya zabuni na maelezo ya huduma na kuiwasilisha kwa Katibu wa Bodi ya Zabuni, Halmashauri ya Wilaya ya Gairo, S.L.P 40, Gairo, chumba na. 70 kabla ya saa 5:00 asubui siku ya Jumanne Tarehe 14/06/2022. Mwombaji awasilishe nyaraka halisi ya zabuni (**original**) moja na nakala mbili.
9. Zabuni zote zitafunguliwa hadharani mara tu baada ya muda wa mwisho wa kuwasilisha, mbele ya wawakilishi wa wazabuni wanaoamua kuhudhuria katika ufunguzi wa zabuni katika Ukumbi Mdogo wa Halmashauri ya Wilaya ya Gairo.
10. Zabuni zitakazochelewa, sehemu ya zabuni, zabuni zisizofunguliwa katika tukio la ufunguzi wa zabuni, hazitakubaliwa kwa ajili ya kutathminiwa kwa hali yoyote ile.


.....

Susan E Nyanda
Kaimu Mkurugenzi Mtendaji
Halmashauri ya Wilaya
GAIRO.

**KAIMU MKURUGENZI MTENDAJI
HALMASHAURI YA WILAYA GAIRO**